



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA**



**TAARIFA KWA UMMA:
MTIHANI WA USAJILI NA LESENI MWEZI SEPTEMBER 2023**

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni Mamlaka ya kisheria inayosimamia taaluma na wanataaluma ya Uuguzi na Ukunga chini ya sheria (**The nursing and Midwifery Act,2010**).

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania linapenda kuwataarifu Watahiniwa wote waliokidhi vigezo vya kufanya Mtihani wa usajili na leseni wa Uuguzi na Ukunga kuwa Mtihani huo utafanyika Tarehe 7 Septemba 2023 siku ya Alhamisi katika vituo vifuatavyo:

CHUO KIKUU CHA MWANZA (Igoma), CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA ELIMU DAR ES SAALAM (DUCE) na CHUO KIKUU CHA MTAKATIFU YOHANA (ST. JOHN) DODOMA-Kikuyu

Hivyo watahiniwa waliokidhi vigezo wanatakiwa kufika kwenye vituo vya Mitihani walivyochagua Tarehe 6 Septemba, Saa mbili kamili, (2:00)Asubuhi, bila kukosa kwaajili ya maelekezo wakiwa na vifaa vifuatavyo:

Kitambulisho chochote chenye picha ya mtahiniwa, Kalamu Nyeusi, Penseli aina ya HB,Pasport size (2) zenye back ground ya light blue(size 35x35)

Kumbuka:Watahiniwa wote wanatakiwa kuwa nadhifu na kuvaa mavazi yenye staha.

Imetolewa na:

**Ezekiel M. Nyalusi
Afisa Mahusiano
Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania.
29 Aug,2023**